Nuru ya Kiswahili, Juzuu 4(1), Juni 2025:1-25
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru41.0125

# Uchimuzi wa Falsafa ya Ubuntu kama Mhimili wa Falsafa ya Waafrika katika Riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1*

**Stela Faustine**
**Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Dodoma**
stella.faustine@udom.ac.tz

## Ikisiri

Makala hii inalenga kujadili namna Falsafa ya Ubuntu inavyojichomoza kama mhimili wa Falsafa ya Waafrika katika riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1*. Utafiti uliozaa makala hii ulikuwa wa kimaktaba. Mbinu ya uchambuzi matini ilitumika katika ukusanyaji wa data. Data zilizokusanywa zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Nadharia ya Epistemolojia imetumika katika mchakato mzima wa ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishwaji wa data. Makala inabainisha namna Falsafa ya Ubuntu inavyojitokeza kama mhimili wa Falsafa ya Waafrika kupitia miktadha mbalimbali ya maisha ya Waafrika. Miktadha hiyo ni: muktadha wa kufanya uamuzi binafsi na wa jamii nzima, muktadha wa ushirika katika kufanya shughuli mbalimbali za kijamii kama vile matatizo na sherehe, pamoja na muktadha wa kimahusiano baina ya mtu na jamii yake. Kwa kuzingatia mjadala uliofanywa, inapendekezwa kuwa tafiti zaidi zifanywe ili kubaini Falsafa Jumuifu ya Waafrika. Hii ni kwa sababu, mpaka sasa Falsafa ya Waafrika imekuwa ikitazamwa kupitia vipengele mbalimbali vya maisha ambavyo vinaibua mitazamo mbalimbali inayobainisha fikra za Waafrika kwa namna wanavyoutazama ulimwengu wao. Mitazamo hiyo, kwa mujibu wa makala hii, inaibua Falsafa 'za' Waafrika zinazoibuka kutoka katika kila kipengele na si Falsafa 'ya' Waafrika kama inavyotarajiwa kuwa.

**Dhana za Msingi**: epistemolojia, falsafa, falsafa ya Waafrika, Ubuntu, falsafa ya Ubuntu

## Utangulizi

Falsafa ni dhana ngumu kuitolea maana inayojitosheleza kiasi cha kurejelewa kwa namna moja katika vipindi na miktadha tofauti. Kwa miongo kadhaa, mijadala kuhusu falsafa imekuwa ikigonga ndani ya vichwa vya wataalamu mbalimbali. Katika mijadala hiyo, wataalamu kama vile Chuachua (2016) na Kavishe (2019) wamefafanua maana ya falsafa kulingana na mwelekeo na madhumuni ya mjadala husika. Mitazamo ya kiwakati na ukuaji wa urazini wa kibinadamu umekuwa ni kichocheo kikubwa cha mabadiliko ya kijamii, hivyo kusababisha mabadiliko ya urazini wa mwanadamu kwa namna anavyoyatazama mambo katika maswala mbalimbali ya maisha. Mabadiliko na upeo wa kimaisha vimesababisha kuwapo kwa mitazamo tofauti kuhusu maana na mitazamo mbalimbali ya kifalsafa. Hii ndiyo sababu inayotulazimu kufafanua dhana ya falsafa kwa mitazamo ya wataalamu mbalimbali, kisha kuja na mtazamo jumuifu wa namna dhana hii itakavyorejelewa katika makala hii.

Durant (1953) anaeleza maana ya falsafa kwa kuihusisha na taaluma ya sayansi aipatayo mtu. Kwa mtazamo wake, falsafa ni taaluma inayojihusisha na upembuzi wa kila kitu kinachomzunguka mwanadamu katika ulimwengu wake. Naye Omari (1980) anaeleza kuwa falsafa ni hekima inayoonesha jinsi tunavyoishi kwa kutenda, kusema na kutosema kwenye kuutafuta ukweli kuhusu jambo fulani katika maisha kwa njia ya kutafakari. Tukiangalia maana za wataalamu wote wawili, tunaona msingi wa mawazo yao unakamilishana katika dhana ya kuutafuta ukweli wa maisha. Hata hivyo, maana hizo zinakuwa na mwachano katika namna ya kuutafuta ukweli. Wakati Durant (*ameshatajwa*) anaamini kuwa ukweli hupatikana kwa misingi ya kitaaluma inayozingatia nduni za kisayansi,

Omari (*ameshatajwa*) anaamini kuwa ukweli uko katika hekima zinazopatikana ndani ya urazini wa mwanadamu.

Wamitila (2016) na Faustine (2017) wanadai kuwa falsafa ni mfumo wa mawazo au fikra ambao humwongoza mwanadamu katika kuishi kwake kulingana na misingi iliyopo. Wataalamu hawa wanaamini kuwa ingawa falsafa inakusudiwa kuutafuta ukweli wa maisha, njia za kuuendea ukweli huo hutegemea misingi iliyopo katika jamii inayohusika. Mtazamo wao unatokana na ukweli unaoelezwa na Chuachua (2016) kuwa njia za kupata maarifa (kuutafuta ukweli) hutofautiana baina ya jamii moja na nyingine. Zipo jamii, kama vile jamii za Kimagharibi, zinaamini kuwa maarifa hupatikana katika taaluma kwa misingi ya kisayansi. Aidha, jamii za Kiafrika huamini kuwa maarifa na ukweli wa jambo hupatikana katika hekima kutoka kwa wazee na wahenga. Kwa vile makala hii inahusiana na Falsafa ya Waafrika, mjadala wake unajiegemeza katika maana zilizotolewa na Wamitila (2016) na Faustine (2017). Maana hizo zinatoa mwanya wa kuyatafiti maarifa kwa kuzingatia misingi ya kiepistemolojia ya jamii husika. Aidha, Falsafa ya Waafrika inatazamwa hapa kuwa ni mitazamo au fikra za Waafrika zinazofungamana na maisha yao. Fikra hizo huaminiwa kuwa zina ukweli fulani unaoongoza maisha ya Waafrika kwa kuzingatia misingi yao ya kiidili.

Falsafa imegawanyika katika matawi mbalimbali. Miongoni mwayo kama yanavyotajwa na Obenga (2004) ni metafizikia, mantiki, epistemolojia na maadili. Ubuntu, kama mhimili wa Falsafa ya Waafrika, unajichomoza kutoka tawi la maadili ambalo linajihusisha na fikra kuhusu mwenendo na utendaji ambao hudhihirika kupitia utamaduni wa jamii husika. Kwa vile makala hii inahusu udhihirikaji wa Falsafa ya Ubuntu kama mhimili

unaoibua Falsafa ya Waafrika, mjadala umefanywa kwa mwegamo wa kiepistemolojia. Ponera (2023) anafafanua kuwa msingi mkuu wa epistemolojia ni kuchambua na kutathmini maarifa katika jamii mbalimbali. Kwa kuwa namna za kuyafikia maarifa hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine (Ponera, *ameshatajwa*), ni wazi kuwa Waafrika wana namna yao ya kufikiri na kuutazama ulimwengu wao, tofauti na namna za jamii nyingine. Katika muktadha huu, makala hii inabainisha namna Falsafa ya Ubuntu inavyosawiriwa kama mhimili wa Falsafa ya Waafrika kwa kuzingatia misingi ya epistemolojia ya Kiafrika.

Ubuntu ni dhana ambayo imekuwa ikiongelewa katika mitazamo tofauti na watafiti na wataalamu mbalimbali. Wapo wanaoitazama dhana ya ubuntu kwa kuihusianisha na asili ya neno Bantu. BAKITA (2017) linaeleza kuwa ubuntu ni uhusiano wa kiuzawa wa watu wanaoongea lugha zenye asili moja ya familia. Wanaendelea kufafanua kuwa lugha ya Nija-Kongo kama vile Kiswahili, Kisukuma, Kikuyu, Kibuganda, Kinyarwanda, Kirundi, Kizulu na Kikhosa ni miongoni mwa lugha zinazojumuishwa katika kundi la lugha za Kibantu. Uhusiano huo unaothibitika kupitia mifumo sawa ya lugha ndio unaowafanya kujiona wamoja, wanaoendesha maisha yao kwa kufuata misingi ya kifalsafa inayofanana (Kagame, 1956; Tempels, 1959; Gyekye, 1995 & Faustine, 2017).

Mtazamo mwingine unafafanuliwa na Ramose (2002). Huyu, anaeleza maana ya neno ubuntu kwa kutazama etimolojia ya neno hilo kuwa limetokana na muunganiko wa dhana mbili ambazo ni kiambishi awali *ubu-* pamoja na mzizi wake *-ntu*. Kiambishi awali *ubu-* kimesimama kama kiwakilishi cha dhana ya ujumla; na *-ntu* ni mzizi ambao unasimama kama kirejeleo cha mtu. Kwa maana hiyo, tunaweza kusema kuwa dhana ya

ubuntu inasimama katika kueleza utu wa mtu au ubinadamu wake. Chuachua (2016) anarejelea mawazo ya Ramose (2002) kwa kusisitiza kuwa ubu-ntu ni nguzo ya fikra za Wabantu kuhusu ontolojia na epistemolojia yao. Fikra hizo zimekita misingi yake katika kusawiri umoja na undugu wa Wabantu kwa namna wanavyofikiri kuhusu ontolojia na epistemolojia yao.

Kwa kuzingatia mtazamo wa ubu-ntu kama unavyofafanuliwa na Ramose (2002) na Chuachua (2016), Waafrika wana imani kuwa "mtu si mtu bila watu". Hii ina maana kuwa ukamilifu wa mtu hautafsiriwi kutokana na ubinafsi wa mtu, bali kwa kuangalia mtazamo, namna ya ushiriki wake kwa jamii nzima, au kwa namna anavyowatendea watu wengine wanaomzunguka. Mtazamo huu unadhihirika katika muundo wa jamii ambao ni wa kutegemeana, pamoja na semi mbalimbali ambazo zinajitokeza katika jamii ya Wabantu. Louw (h.t.) anafafanua kuwa Wazulu wanaopatikana Afrika Kusini wanasema: *Umuntu ngumuntu ngabantu* wakiwa na maana ya mtu si mtu bila watu. Aidha, Wahaya wanaopatikana nchini Tanzania wanasema: *Omuntu ti muntu ka ataliho bantu* wakiwa na maana ya mtu si mtu kama hakuna watu. Kimsingi, semi hizi zinabainisha mtazamo wa Waafrika kuhusu Falsafa ya Ubuntu ambayo msingi wake mkuu uko katika mtazamo wa U-SISI (upamoja) na sio U-MIMI.

Kwa mujibu wa Prinsloo (1995), Falsafa ya Ubuntu hujipambanua katika misingi ya umoja, huruma, heshima, uvumilivu na upendo. Hata hivyo, misingi yote hiyo inakitwa katika mfumo wa ushirika ambao unaitazama thamani ya utu wa mtu kwa namna anavyowatendea watu wengine. Faustine (2017) anaeleza kuwa miongoni mwa sababu za kuwapo kwa mtu na ukamilifu wake katika jamii za Kiafrika ni umoja. Anaongeza kuwa, kwa

Waafrika, utu wa mtu hukitwa katika imani ya kuwapo kwa nguvu hai. Nguvu hizo zinatokana na namna mtu anavyoishi, kutii na kuzingatia mitazamo na maadili ya jamii yake. Kwa Waafrika, mtu yuko katika ukamilifu wake kwa sababu ya kuwapo kwa watu wengine. Duara hili la kuwapo haliwajumuishi walio hai peke yao, bali pia waliokufa (mizimu) na miungu.

Falsafa ya Ubuntu imekuwa ikitazamwa kwa ujumla kama kipengele cha Falsafa ya Waafrika. Jambo hili linafanya falsafa hii kupwaya kutokana na kukosekana kwa utambuzi wa maarifa iliyobeba kama mhimili wa Falsafa ya Waafrika. Kagame (1956) anabainisha kuwapo kwa lugha za Waafrika zenye mfumo unaofanana. Mfumo huo husawiri fikra, maarifa na mitazamo kuhusu maisha ya Waafrika. Maarifa yanayopatikana katika andiko hilo yanatufanya kujenga hoja kuwa msingi mkuu wa Falsafa ya Waafrika unatokana na mfumo wa lugha unaofanana. Licha ya andiko la Kagame (*ameshatajwa*) kuweka msingi mzuri wa kiuelewa kuhusu Falsafa ya Waafrika, tunaona kuwa halijabainisha namna Falsafa ya Ubuntu inavyosimama kama mhimili wa Falsafa ya Waafrika. Mawazo ya Kajosi (2013) yanakinzana na ya Kagame (*ameshatajwa*) kuhusiana na mhimili mkuu unaoijenga Falsafa ya Waafrika. Anaona kuwa msingi mkuu wa fikra za Waafrika umekitwa katika suala la uzazi. Hoja ya msingi hapa ni kuwa uzazi ndio chanzo cha kuwako kwa mwanadamu na ulimwengu wake. Hivyo fikra zote zinazojengwa kuhusu Falsafa ya Wafrika, zinaanzia katika suala la kuwako kwake. Tempels (1959) na Faustine (2017) wanaona kuwa maisha ya Waafrika yanatangamana na nguvu hai. Wanatoa ufafanuzi kuwa nguvu hii ndiyo hutoa mtazamo yakinifu wa maisha ya Waafrika. Faustine (*ameshatajwa*), mathalani, anasema kuwa Falsafa ya Waafrika ambayo

hudhihirika kupitia vipengele mbalimali vya maisha imejengwa katika msingi wa falsafa kuu ya kuwapo kwa nguvu hai. Baadhi ya vipengele hivyo ni imani kuhusu uzazi, ulezi, thamani ya mtu na utu wake, thamani ya roho, uhai na kifo, ulimwengu wenye matabaka, umoja, uduara, wakati, pamoja na hekima (Griaule, 1965; Oruka, 1990; Chuachua, 2016; Kavishe, 2019; Faustine, 2023; na Ponera, 2023).

Kimsingi, maoni ya wataalamu waliotajwa kuhusu mhimili unaosimama kama kijenzi cha Falsafa ya Waafrika yamekuwa kichokoo kikubwa kilichoibua maswali ya msingi yaliyoamsha ari ya kufanyika kwa utafiti uliozaa makala hii. Nayo ni: je, mhimili mkuu wa Falsafa ya Waafrika unaoitofautisha na falsafa ya jamii nyingine ulimwenguni ni upi? Je, ni maarifa gani ya msingi yanayotazamwa kuwa ndio kibainishi jumuifu cha Falsafa ya Waafrika? Maoni ya makala hii ni kuwa Falsafa ya Waafrika ambayo inabainisha fikra kuhusu namna wanavyoendesha maisha yao hudhihirika kupitia falsafa ya Ubuntu. Falsafa hii imekitwa katika msingi mkuu wa umoja. Vijenzi vya msingi huu ni utu, wema, haki, ukarimu, na upendo. Kwa mujibu wa Shutte (1993), falsafa ya Ubuntu humtazama mtu kama sio kamili katika U-MIMI bali U-SISI. Ushirika huu wa kiuhusiano hauwahusu walio hai peke yao, bali huwajumuisha pia waliokwishakufa (Ndaba, 1994; Van Niekerk, 1994).

Imekwishaelezwa hapo awali kuwa falsafa ya Ubuntu hujichomoza kutoka katika tawi la falsafa la kimaadili. Kwa vile tawi hili linajihusisha na fikra kuhusu mwenendo na utendaji ambao hubainika kupitia utamaduni wa jamii husika, data za makala zilikusanywa kutoka riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1.* Kama inavyoelezwa na wataalamu kama Madumulla (1988), na Mlacha (1996), riwaya hii ina

utajiri wa utamaduni wa Mwafrika. Hivyo basi, kwa upeo wa mapitio yaliyofanywa na mwandishi, ilionekana kufaa kutumika kama chanzo cha upatikanaji wa data zilizozalisha makala hii. Hii ni kwa sababu inaakisi misingi ya kifalsafa ya jamii ya Waafrika inayodhihirika kupitia maudhui yanayojitokeza ndani yake.

## Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ya Epistemolojia iliongoza utafiti uliozaa makala hii. Pia, imetumika katika mjadala wa makala. Stumpf & Abel (2002) wanaeleza kuwa epistemolojia ni neno lenye asili ya Kiyunani ambalo limetokana na muunganiko wa maneno mawili, yaani *episteme* (maarifa) na *Logos* (neno). Chuachua (2016) anafafanua kuwa Epistemolojia ni tawi la falsafa linaloshughulika na tafakuri kuhusu wapi maarifa yanaweza kupatikana, namna gani ya kupata maarifa hayo na mawanda ya upatikanaji wake. Akifafanua dhana ya epistemolojia kwa kuifungamanisha na kazi za fasihi, Faustine (2017) anaeleza kuwa hii ni dhana inayohusiana na utambuzi unaomwezesha mtu au msomaji wa kazi za fasihi kupata maarifa au ujuzi wa jambo fulani. Hata hivyo, pamoja na kuwa epistemolojia ni tawi la falsafa, Kasprisin (1987) anafafanua kuwa ni umbo lenye misingi kamili na dira mahususi inayoweza kutumika kama nadharia ya uhakiki wa kazi za fasihi. Newman (2023) anaeleza kuwa René Descartes ndiye mwasisi wa Nadharia ya Epistemolojia. Inaelezwa na Cottingham (2010) kuwa René Descartes alifanya mageuzi makubwa kwa kupanua mawanda ya kimtazamo kutoka kuitazama epistemolojia kama dhana na tawi la falsafa na kuiona kama nadharia ya maarifa inayoweza kutumiwa kama nyenzo ya kuchambulia masuala mbalimbali ya kimaisha.

Ifuatayo ni misingi ya Nadharia ya Epistemolojia iliyotumika katika uchambuzi wa data za makala hii: Mosi, mawazo, tajriba na mitazamo ambayo ni chanzo cha maarifa inaweza kupatikana pia katika vyanzo vya kihistoria pamoja na masimulizi ya kifasihi (Chuachua, 2016). Pili, maarifa hutokana na ujuzi wa mtu anaoweza kuupata kutokana na tajiriba ya maisha yake (Chuachua, 2016; Faustine, 2017). Tatu, namna ya upatikanaji wa maarifa hutofautiana baina ya jamii moja na nyingine. Waafrika huamini kuwa vyanzo vya maarifa hutoka kwa wahenga na wazee wenye umri mkubwa (Ponera, 2023) na kwa jamii za Ulaya maarifa hupatikana kwa tabasuri, usanisi na tajiriba. Tabasuri husisitiza upatikanaji wa maarifa kwa kutumia akili, na usanisi ni matokeo ya ushirika wa hisia na akili (Stumpf & Abel, 2002). Nne, maarifa ni mali ya jamii (Ponera, 2023).

Misingi hii ilisaidia katika uchambuzi wa data na mjadala wa makala: Msingi wa kwanza ulimwezesha mtafiti kuchagua riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1* ili kupata data za msingi zinazohusiana na jamii ya Waafrika. Hii ni kwa sababu riwaya hii ambayo inasawiri maisha ya jamii ya Waafrika (hivyo kuhifadhi utamaduni na falsafa ya jamii ya Waafrika) ilionekana muafaka katika mjadala wa makala hii. Msingi wa pili na wa tatu imesaidia kupatikana kwa maarifa kama inavyosadikiwa na jamii ya Waafrika. Pia, imewezesha kubaini fikra na mitazamo ya Waafrika kuhusu falsafa ya Ubuntu kwa kuzingatia namna ya uwazaji wao uliokitwa katika misingi ya utu, umoja na mshikamano wa kindugu. Msingi wa nne umetoa mwanga wa kimaarifa kuwa fikra za Waafrika zimekitwa katika misingi ya umoja na sio ubinafsi. Kwa ujumla, msingi huu unatoa picha ya jumla ya Falsafa ya Ubuntu inayokitwa katika dhana ya U-USISI na sio U-MIMI.

## Methodolojia

Utafiti uliozaa makala hii ulisanifiwa kifenomenolojia, hususani fenomenolojia ya kihemenitiki. Kwa mujibu wa Ponera (2019), aina hii ya usanifu huhitaji fikra za mtafiti katika kusaka maana kutokana na data zilizokusanywa. Data za utafiti huo uliotumia mkabala wa kitaamuli zilikusanywa maktabani kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa maandiko. Data za msingi zilipatikana kutoka riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1*. Mbinu ya usampulishaji lengwa ndiyo iliyotumika katika kuteua riwaya hiyo. Hii ni kwa sababu maudhui ya riwaya hiyo yanaendana na mada husika. Data za upili zilipatikana kutoka katika maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada husika. Kwa kuongozwa na misingi ya Nadharia ya Epistemolojia, data zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui.

## Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti. Imeundwa na vijisehemu viwili: maelezo mafupi ya ufafanuzi kuhusu riwaya teule pamoja na ufafanuzi kuhusu namna falsafa ya Ubuntu inavyojichomoza kama mhimili wa Falsafa ya Waafrika katika riwaya teule.

### Maelezo mafupi kuhusu riwaya teule

*Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1* ni riwaya iliyotungwa na Aniceti Kitereza. Awali, riwaya hii iliandikwa kwa lugha ya Kikerewe[1] ambayo ndiyo lugha mama ya mwandishi. Baadaye aliitafsiri yeye mwenyewe kwenda lugha ya Kiswahili. Riwaya hii ilichapishwa mwaka 1980 na Tanzania Publishing House. Iko katika juzuu

[1] Hii ni lugha ya jamii ya Wakerewe ambao wanapatikana katika Kisiwa cha Ukerewe. Kisiwa hicho kimo katika Ziwa Viktoria.

mbili. Juzuu ya kwanza inahusiana na maisha ya Myombekere na mkewe, Bugonoka. Juzuu ya pili ni mwendelezo wa juzuu ya kwanza, ambapo Kitereza anasimulia maisha ya mtoto wa Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka aitwaye Ntulanalwo. Mjadala wa makala hii umefanywa kwa kumakinikia maudhui yanayopatikana ndani ya juzuu ya kwanza tu. Juzuu hiyo imegawanyika katika sura kumi na nane (18) ambazo zinajadili changamoto mbalimbali za maisha wanazokabiliana nazo Myombekere na Bugonoka baada ya kukosa mtoto kwa muda mrefu katika ndoa yao. Licha ya misukosuko ya kijamii inayochagizwa na tamaduni za Kiafrika zinazoamini kuwa mtoto ni msingi wa ndoa na kiini cha mwendelezo wa maisha, wawili hao wanapambana kwa hali na mali; mwisho, wanabarikiwa kupata mtoto wa kiume ambaye ni Ntulanalwo.

## Miktadha inayodhihirisha Ubuntu kama mhimili wa falsafa ya Waafrika

Imebainika kuwa Ubuntu ni falsafa ambayo msingi wake umekitwa katika fikra za U-SISI wa kiutegemezi. Katika muktadha wa makala hii, hii ni falsafa inayotazamwa kuwa kitovu cha fikra za Waafrika kwa namna wanavyoyachukulia na kuyaendesha maisha yao. Wataalamu kama vile Kagame (1956), Tempels (1959), Gyekye (1995) Mbiti (2011) na Kajosi (2013) wanabainisha vipengele mahususi ambavyo huchukuliwa kuwa huibua maarifa mbalimbali yanayobainisha Falsafa ya Waafrika. Licha ya kuwapo kwa vipengele hivyo, bado Falsafa ya Ubuntu inasimama kama mhimili wa mitazamo ya Falsafa ya Waafrika inayoibuliwa kwavyo. Hii inamaanisha kuwa msingi wa mafanikio katika utekelezaji wa jambo lolote katika jamii ya Waafrika huegemezwa katika duru ya umoja ambayo inajifungamanisha na muundo wa jamii.

Kwa mujibu wa Mlacha (1996), riwaya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu na. 1* imeandikwa katika muundo ambao ni muhimu katika kueleza muktadha wa utamaduni wa jamii husika. Muundo huu unaonesha uhusiano baina ya mtu, utamaduni unaomzunguka na muundo wa jamii, kiasi cha kuthibitisha kwamba mtu si sehemu tu ya jamii yake bali pia ni sehemu muhimu katika kuikamilisha jamii hiyo. Uhusiano huu wa kiutegemezi unaobainika kupitia desturi za Waafrika ndio unaoibua fikra za kibuntu ambapo kwazo, mtu hutazamwa katika ukamilifu wake katika duara pana linalodhihirisha mahusiano ya umoja katika kijamii. Uhusiano huu unadhihirika katika muktadha wa kufanya uamuzi, muktadha wa ushirika katika shughuli za kijamii pamoja na muktadha wa uhusiano baina ya mtu na jamii.

***Muktadha wa kufanya uamuzi***

Waafrika huamini kuwa suala la kufanya uamuzi halichukuliwi katika mtazamo binafsi, bali huhusisha jamii nzima. Hii ni kwa sababu mtu hawezi kukamilika katika upekee wake pasipo kuhusishwa na muundo au kwa kujitenga na muundo wa jamii yake.

Imani na mtazamo wa jamii nzima, kulingana na fikra za Waafrika, vina athari kubwa katika mtazamo wa mtu binafsi. Hali hii inajitokeza katika suala zima la uzazi ambapo Waafrika wanaamini kuwa si jambo linaloweza kufanyiwa uamuzi na wazazi peke yao, bali jamii nzima. Mbiti (2011) anaeleza kuwa, kwa Waafrika, uzazi unatazamwa katika hali endelevu kuanzia katika hatua ya mimba ambapo mama hupewa uangalizi maalumu na jamii mpaka pale mtoto anapozaliwa. Hali hiyo huendelea pia katika suala la makuzi ya mtoto huyo. Mbiti (*ameshatajwa*) anasisitiza kuwa Waafrika huamini kwamba asili ndiyo inayowatunuku wanandoa mtoto.

Hata hivyo, majukumu ya kumlea mtoto huyo (ambalo huanzia akiwa tumboni), kumlinda, na kumjenga kama mshirika mzuri wa jamii yake ni la jamii nzima.

Kupitia riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1*, mwandishi anaonesha namna suala la uzazi linavyoamuliwa na wanajamii. Anasema:

> Hapo jamaa wa Myombekere wakaanza kuwaka hasira na kupayuka wakimwambia amkatae mke wake, wakisema 'wewe ni ndugu yetu, sasa unakubali kweli kukaa na mke wako huyu akiwa mgumba hivi? Uzuri wako huo wote uishie chini! Hivi wewe unadhani kufufuka kwa watu hapa duniani ni nini? Si kuzaa na kuacha mbegu yako ikiwa hai ndio maendeleo ya ukoo wetu? Kama wewe baba yako na mama yako wasingekuzaa ungetoka wapi? (uk.1).

Chimbuko la fikra ya kwenye nukuu hii ni tatizo la kukosa mtoto lililomo katika ndoa ya Myombekere na mkewe, Bugonoka. Ijapokuwa kwa mtazamo wa kawaida ndoa huonwa kama jambo la wanandoa wawili, tunaona namna jamii inavyosimama kidete na kuchukua uamuzi wa namna ya kulitatua. Jamaa wa Myombekere wanamshurutisha aachane na mkewe na kuoa mwanamke mwingine ili aweze kupata watoto. Kwa ujumla, nukuu inatumulikia kuwa suala la uzazi kwa jamii za Waafrika halitazamiwi kuwa jukumu la wanandoa peke yao, bali la jamii nzima. Kitendo cha ndugu wa Myombekere kufanya uamuzi kwa niaba yake, na kumwambia amkatae mkewe, ni kibainishi cha ushirika uliojengwa katika jamii za Waafrika. Ushirika huo unasimama kama mhimili wa imani inayoongoza maisha yao kuwa msingi mkuu wa ndoa ni mtoto (Kajosi, 2013 na Faustine, 2017). Pia, mtoto ndiye kiunganishi cha familia baina ya mke na ndugu wa mume. Hatimaye, mtoto humfanya mke kukubalika katika duara kubwa la ukoo.

Haya yote ndiyo huifanya jamii kuutazama uhusiano wa ndoa katika misingi ya udugu na umoja.

Tatizo la Bugonoka kutoshika ujauzito linasababisha wazazi wake kuchukizwa na masimango na lawama ambazo binti yao anatupiwa na ndugu wa Myombekere. Wanaichukulia aibu anayoipata binti yao kama aibu ya familia. Kutokana na kadhia hiyo, wanafanya uamuzi wa kuvunja ndoa yake na kumrudisha nyumbani kwao pasipo ridhaa yake. Muundo wa kijamii unaojikita katika mihimili ya falsafa ya Ubuntu ndio unaochagiza uamuzi wa wanandoa hao kufanywa na wazazi. Kwa vile suala la ndoa—kuanzia kumchagua mchumba mpaka taratibu zote katika ukamilifu wake—hutazamwa kijamii (Mbiti, 2011), Waafrika huamini kuwa hata uamuzi wa kuvunja au kurekebisha ndoa endapo itaonekana kuwa na migogoro sio suala la wanandoa peke yao, bali hutazamwa kijamii kuanzia ngazi ya familia. Katika riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1*, mtazamo huu wa ushirika katika kufanya uamuzi kuhusu jambo lolote linalohusiana na masuala ya ndoa unajitokeza pale Bugonoka anapokataa kurudi nyumbani kwake kwa kusema:

> … mimi sina makuu mengi, wazee wangu ndio walionioza kwako na ndio walioudhika na kuumwa sana juu ya matusi yenu hayo. Lakini kwa utashi wao wazazi wangu wangekwisha kunioza … (uk. 18)

Katika nukuu hii, falsafa ya Ubuntu imejitokeza kwa mwegamo wa msingi wa umoja inavyochukua nafasi kama mhimili wa falsafa ya Waafrika. Nukuu inabainisha kuwa suala zima la kufanya uamuzi kuhusiana na ndoa sio jukumu la Bugonoka peke yake. Mtazamo huu unatokana na imani iliyojengeka kutokana na muundo wa jamii kuwa licha ya Bugonoka kuwa mke, bado anatazamwa kama mtoto, dada, shangazi na kama mwanajamii.

Hivyo basi, jambo lolote analokabiliana nalo, jema au baya, huigusa jamii kwa namna mbalimbali. Hivyo basi, kwa desturi za Waafrika, msamaha wa Myombekere haupaswi kuridhiwa na Bugonoka peke yake, bali na jamii nzima kwa namna mbalimbali. Wanaepistemolojia wanaamini kuwa hekima hutokana na ujuzi alionao mtu anaoweza kuupata kutokana na tajiriba ya maisha yake. Mtazamo huu unaturejesha kwenye muundo wa jamii wa upamoja unaoibua falsafa ya Ubuntu. Muundo huo huwaweka wanajamii katika ushirika wa kiuamuzi kwa misingi ya kutegemeana. Hii inasababishwa na hoja kuwa, ni katika jamii ndiko kuliko na watu wenye hekima inayotokana na uzoefu wa maisha kulingana na umri walionao; hivyo wanasadikiwa kuwa na uamuzi wenye hekima katika masuala mbalimbali ya kimaisha.

Falsafa ya Ubuntu kama mhimili wa Falsafa ya Kiafrika inadhihirika pia katika suala la uongozi. Katika riwaya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1*, tunaoneshwa kuwa licha ya jamii ya Myombekere kuwa na kiongozi anayepaswa kusimamia kila kitu na kutoa uamuzi mbalimbali unaohusiana na jamii yake, bado fikra za Waafrika kuhusu kufanya na kuamua jambo kwa pamoja zinamfanya kiongozi huyo aone haja ya kuishirikisha jamii yake. Mwandishi anabainisha hili kwa kusema:

> … Sasa mimi ninataka waseme kesi yao mbele yenu, msikilize na kuiamua, ndio maana nimewazuia msiendelee kupiga kelele, nikisema, *enzoga tesiga kigambo*!'' (mahali palipo na pombe, hapafichi siri!) (uk.31 – tafsiri kwenye mabano ni ya mwandishi wa riwaya hii) (uk. 31).

Nukuu hii inahusu tukio la Ntamba kumshtaki Myombekere kwa Jumbe kufuatia ng'ombe wa Myombekere kula mazao yake. Anapoipata kesi hii,

Jumbe anaiwasilisha kwa wanajamii ili washiriki kufanya uamuzi wa pamoja.

Wanaepistemolojia wanaamini kuwa namna ya upatikanaji wa maarifa hutofautiana baina ya jamii moja na nyingine. Hivyo, kwa Waafrika, maarifa hutoka kwa wahenga na wazee wenye umri mkubwa. Aidha, maarifa si mali binafsi ya mwanajamii, bali ni mali ya jamii nzima. Katika muktadha huu, ni dhahiri kuwa uamuzi wa Jumbe kuwashirikisha wanajamii kufanya uamuzi wa pamoja umetokana na imani ya Waafrika kuwa maarifa yanapatikana kwa wanajamii wenyewe kwa misingi ya umoja. Kwa Waafrika, kiongozi mzuri au mtu mzuri ni yule anayewasikiliza wengi na kukubalika na wengi. Zipo semi mbalimbali ambazo zinabainisha imani ya Waafrika kuhusu suala la umoja katika utatuzi wa masuala mbalimbali. Methali kama vile 'mkataa wengi ni mchawi', 'penye wengi pana mengi' na au 'penye wengi hapaharibiki neno' zinabainisha misingi ya falsafa ya Waafrika ambayo imejengwa katika swala la umoja.

Katika mwendelezo wa usimulizi wa mgogoro wa Myombekere na Ntamba, mwandishi anaonesha zaidi namna uamuzi wa pamoja unavyotawala maisha ya Waafrika. Hili analionesha kupitia utayari wa wanajamii katika kushirikiana na Jumbe ili kutatua mgororo huo. Katika kuitikia rai ya kiongozi wao juu ya mgogoro huo, wanajamii wote waliohudhuria kikao hicho walijibu kwa pamoja: "Ndiyo bwana Jumbe, hayo ndiyo sawa, na sisi tunapenda wayaseme tuyasikie sote, sababu kila mara hapa nchini shauri huamuliwa hadharani kwenye watu wengi" (uk. 32). Baada ya mawazo ya watu mbalimbali kuhusiana na shauri la Myombekere na Ntamba, Jumbe

anakata shauri kwa kukita uamuzi wake kwenye mawazo ya wengi kwa kusema:

> Hata mimi yaliyosemwa na watu mashuhuri na hata raia nimeyapokea sawasawa. Basi, nikate kesi sasa: Ntamba, umeshindwa sharia, sababu kesi kila mara huamuliwa na watu wengi. Kisa ni kwa sababu ya kumpiga vibaya sana mtoto wa Myombekere, kama mtoto huyu hangeokolewa na mguu wake, angekufa (uk. 36).

Nukuu hii inabainisha mtazamo wa wanaepistemolojia wanaoamini kuwa, kwa Waafrika, maarifa ni mali ya jamii. Hivyo, uamuzi wa mwisho unaotolewa na Jumbe kwa kuzingatia mtazamo wa watu wengi kuhusiana na kesi hiyo unabainisha fikra na mtazamo wa Waafrika. Zaidi, namna hiyo ya kufikia uamuzi inatuonesha kuwa Waafrika hulitazama suala la ushirika wa kiuamuzi kama njia bora ya utatuzi wa matatizo na masuala mbalimbali ya jamii. Hii inatokana na imani iliyojengeka katika fikra zao kuwa penye wengi pana mengi. Hivyo, utatuzi wa jambo lolote katika ushirika huhusisha watu mbalimbali wenye maarifa tofauti. Mseto huo wa maarifa huweza kusaidia kutatua jambo kwa urahisi, kuliko linapofanywa na mtu binafsi.

### *Muktadha wa ushirika katika shughuli za kijamii*

Muktadha mwingine ambamo falsafa ya Ubuntu inajitokeza kama mhimili wa Falsafa ya Waafrika unahusiana na utekelezaji wa mambo mbalimbali ya kijamii kama vile sherehe, misiba na migogoro inayohusu uhusiano. Onyedinma & Kanayo (2013) na Duwe (2022) wanabainisha hili kwa kusema kuwa Waafrika ni jamii ambayo maisha yao yamekitwa katika misingi ya ushirika katika utekelezaji wa masuala yanayohusiana na huzuni na furaha. Mtazamo wa wataalamu hawa unabainisha imani ya Waafrika kuwa umoja ndio msingi wa utatuzi na mafanikio ya jambo lolote katika

jamii. Pia, ni kipimo cha thamani ya mtu na utu wake. Kwa Waafrika, mtu atatambulika kuwa ana utu na upendo kwa wenzake kwa namna anavyoshiriki katika maswala mbalimbali ya kijamii na sio yake binafsi. Katika riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1*, mtazamo huu wa kifalsafa unasimama kama mhimili wa falsafa ya Waafrika kupitia mhusika Myombekere. Tunaoneshwa kuwa, baada ya kupewa adhabu ya kutengeneza pombe na wakwe zake, anashirikiana na watu mbalimbali, akiwamo rafiki yake, Nkwezi, na familia yake, ili kuikamilisha. Mwandishi anatujulisha:

> Walipofika kule, wakazikuta ndizi madhubuti hasa. Basi, wakajitutumua kuzichukua, wanaume kwa wanawake na watoto wao. Yule mtoto mdogo mwanamume pamoja na wanawake wakachaguliwa ndizi zinazoweza kuchukuliwa moja moja; wakatengeneza kata zao na kujitwika. Vijana wakubwa wakafungia ndizi sita katikati ya mti wao, wakazipeleka kwa uchovu mwingi, wakitokwa jasho, hadi penye *embiso* (shimo la kuvumbikia ndizi za pombe)… Na wazee wao nao walichukua zaidi kuliko watoto wao! Walipohesabu wakaona kuwa kwa safari moja wamechukua ndizi kumi na tano (uk. 70 – ufafanuzi wa kwenye mabano ni wa mwandishi wa riwaya katika sherehe).

Licha ya kuwa tatizo la ndoa yake linagusa maisha yake binafsi, jamii haimuachi peke yake. Mwandishi anaonesha kuwa wanajamii hao wanashirikiana bega kwa bega na Myombekere kutengeneza pombe kuanzia hatua ya kuandaa ndizi, kuzisomba, na kuvumbika mpaka pombe ilipokamilika.

Ushirika huu wa kiuhusiano ambao unasimama kama mhimili wa tafsiri ya maisha ya Waafrika hauishii tu katika swala la utengenezaji wa pombe. Tunaona kuwa baada ya pombe kuwa tayari, Myombekere anaipeleka kwa

wakwe zake. Huko kunafanyika sherehe ya kumpokea ambayo inajumuisha jamii nzima. Mwandishi anasema:

> Pitepite wenyeji wakawaona wageni wanafika mjini pale. Hapo wanaume waliokuwa mjini humo, na waliokuwa wamealikwa kuja kunywa pombe hiyo, wakainuka wote kwenda kuwalaki wageni na kuwapokea silaha na mitungi ya pombe. Wanawake waliokuwapo wakashughulika kuwatafutia wageni viti. Wengine wakakimbia kwenda kutafuta viti katika miji ya majirani, kwa sababu pale mjini Namwero hapakuwa na viti vya kuwatosha wageni (uk. 88).

Baada ya kukamilisha adhabu na kupewa mkewe, Myombekere anaamua kushiriki furaha yake na wanajamii wanaomzunguka. Hapa tunaendelea kuoneshwa namna fikra za Ubuntu (zinazokitwa katika misingi ya utu, upendo na ushirikiano) zinavyotawala maisha ya Waafrika katika maswala mbalimbali. Mathalani, hali ya kumkosa mkewe haikuchukuliwa kama tatizo binafsi, bali ni la jamii; ndiyo maana wanajamii walishirikiana naye katika kulitatua. Vilevile, furaha ya kumrejesha mkewe anaitazama kama furaha ya jamii nzima. Kwa namna ileile aliyoshirikiana na wanajamii kumrejesha mkewe nyumbani, anafanya sherehe na kufurahi pamoja nao huku wakinywa na kucheza kwa pamoja. Akisimulia kuhusu wanajamii hao walivyoshirikiana kufurahi, mwandishi anasema:

> Wachezaji wale waliosimama na kurukia uwanjani, wakawahimiza wale waliokaa, na kusema, “Tupigieni makofi, yaani furaha ya ujirani wetu, muone *amafunzo* (matete) ya mtoni *nahubiri* jinsi yanavyopeperusha mabega kwa ufundi sana.” Ee! Pale, makofi yalipasua hewa, kwa kufuatia kipimo cha sauti ya kinanda na mwimbaji mwenyewe. Hapo wachezaji wakaanza kunepa na kupeperusha mabega yao kwa nguvu sana, tena tumbo zao, kusema haki, zilifanana kama hazina matumbo ndani yake… wanawake nao hawakuchelewa kufuatisha vigelegele; ikawa: “Keye! Keye! Keye!” Wanawake walipoona wachezaji wale wakipeperusha mabega yao na miili yao kama kwamba haina

> mifupa ndani mwake, hapo nao wakaanza kupiga vigelegele, na kila mmoja wao alifanya hila yake ya kuvua nyerere miguuni na mikononi ili wapate kuwafichua wachezaji uwanjani… (uk. 112, ufafanuzi wa kwenye mabano ni wa mwandishi wa riwaya)

Uchezaji wa namna hii unayakinishwa na Kiango (1973) anayesema kuwa, kwa Waafrika, uchezaji hufanywa kwa ushirika, na si kipwekepweke. Umoja huu wa kiutendaji ni uthibitisho wa namna Waafrika wanavyoikita miktadha mbalimbali ya maisha yao katika misingi ya kushirikishana na kutegemeana. Masuala yote yanayowazunguka yamejengwa katika uduara ambao hushikiliwa na mhimili mkuu wa falsafa ya Ubuntu.

***Muktadha wa uhusiano baina ya mtu na jamii***

Falsafa ya Ubuntu kama msingi wa Falsafa ya Waafrika inabainika pia kwa namna Waafrika wanavyotafsiri uhusiano baina ya mtu na mtu katika muundo mpana wa kiushirika katika jamii. Tunaona kuwa, licha ya Myombekere kuwa na nafasi ya kiuhusiano ya mtu na mtu kama mkwe, shemeji, mume na mtoto katika familia yake, muundo wa jamii unamfanya kuwa na nafasi hizohizo kwa wanajamii wengine. Mlacha (1996) anafafanua uhusiano huu kwa kusema kuwa muundo wa jamii ambao ni kibainishi cha utamaduni wake unaruhusu mtu huyo kuwa na nafasi maalumu katika jamii yake katika muda wote wa maisha yake.

Katika riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1*, tunaona kuwa uhusiano wa Myombekere kwa mke wake unafungamanishwa na jamii yake. Bugonoka hatazamwi kama mke wa Myombekere tu, bali anatazamwa pia kama mke kwa upande wa familia pamoja na marafiki wa rika lake wanaomzunguka. Mtazamo huu unajenga

ukaribu na kuimarisha utu baina ya wanajamii. Mwandishi anatanabaisha kuhusu hili anaposema:

> … Hapo wenzake Myombekere wakawa wakisemezana kichinichini wao kwa wao: wawili wakizungumza yao, na kadhalika. Halafu wakamuuliza Myombekere, "mbona tunakaa na kuongea peke yetu, je mke wetu Bugonoka yuko wapi?" (uk. 88-89).

Kwa upande mwingine, tunamwona Myombekere hathaminiwi wala kutambulika katika upekee wake kama mkwe ukweni kwake. Falsafa ya Ubuntu iliyojengwa kutokana na muundo wa jamii unaoamini katika misingi ya umoja wa kindugu unawafanya wanajamii kuutazama uhusiano huo kwa mawanda ya jamii nzima. Myombekere hatambuliki kama mkwe kwa familia ya Bugonoka tu, bali kwa jamii nzima inayoizunguka familia hiyo. Pia, familia haimtambui Myombekere peke yake kama mkwe bali inawatambua watu wote wa familia ya Myombekere na jamii iliyomzunguka. Mwandishi anabainisha hili kwa kusema:

> Miongoni mwa waandaaji, alitokea mtu mmoja akawaambia wageni kwa jinsi ya mila ya humu Kisiwani, akasema, "*Iitwe niho twabonera Bakwelima*!" (Pokeeni wakwe zetu, hilo ndilo toleo letu) ...Wakwe nao pia wakamwambia pia hivi, "A, sisi bora mke wetu, baba mkwe!" … (uk. 93 – ufafanuzi wa kwenye mabano ni wa mwandishi wa riwaya).

Katika nukuu hii, dhana ya U-SISI ambayo ni msingi wa falsafa ya Kiafrika inajitokeza wazi kama msingi wa jamii za Waafrika. Vifungu vya '… Wakwe zetu …' na '… Mkwe wetu …' ni ithibati ya namna Waafrika wanavyoamini na kutazama uhusiano kwa kuhusianisha na muundo wa kijamii. Hii ni kaida inayobainisha fikra za Mwafrika kuhusu maswala mbalimbali ya kiuhusiano.

## Hitimisho

Makala hii imejadili falsafa ya Ubuntu kama mhimili unaoibua Falsafa ya Waafrika. Mjadala umebainisha namna falsafa ya Ubuntu inavyojitokeza kama msingi wa Falsafa ya Waafrika kupitia miktadha mbalimbali ya maisha ya Waafrika. Nayo ni muktadha wa kufanya uamuzi, muktadha wa kushirikiana katika kufanya shughuli za kijamii, pamoja na muktadha wa kiuhusiano baina ya mtu na jamii. Makala imefanikiwa kudhihirisha data za hoja hizi kutoka katika riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Buliwhali Juzuu ya 1*. Kwa kuzingatia mjadala uliofanywa, inapendekezwa kuwa tafiti zaidi zifanywe ili kubaini falsafa jumuifu ya Waafrika. Hii ni kwa sababu, mpaka sasa falsafa ya Waafrika imekuwa ikitazamwa kupitia vipengele vya maisha ambavyo vinaibua mitazamo mbalimbali inayobainisha fikra za Waafrika kuhusu ulimwengu wao. Mitazamo hiyo, kwa mujibu wa makala hii, inaibua Falsafa 'za' Waafrika zinazoibuka kutoka katika kila kipengele na si Falsafa 'ya' Waafrika kama inavyotarajiwa kuwa.

## Marejeleo

BAKITA (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili (Tol. 2)*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu* (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Cottingham, J. (2010). Between two Worlds: A Reading of Descartes's Meditations, by John Carriero. *Mind*, 119 (475), 786-789. Inapatikana katika https://doi.org/10.1093/mind/fzq046.

Durant, W. (1953). *The History of Phylosophy: The Lives and Opinions of the Greater Philosophers*. New York: Simon and Schuster.

Duwe, M. (2022). *Uchimuzi wa Eskatolojia ya Waafrika katika Fasihi Simulizi: Mifano kutoka* Mbolezi za Jamii ya Wangoni (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Faustine, S. (2017). *Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili* (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Faustine, F. (2023). Mtazamo kuhusu Wakati katika Falsafa ya Kiafrika: Mifano kutoka Riwaya Teule za Kiswahili. *Nuru ya Kiswahili*, 2(2):1-24.

Griaule, M. (1965). *Conversations with Ogotemmeli: An Introduction to Dogon Religious Ideas*. London: Oxford University Press.

Gyekye, K. (1995). *An essay on African Philosophical Thought: The Akan Conceptual Scheme.* Philadelphia, PA: Temple University Press.

Kagame, A. (1956). *La Philosophie Bantu-Rwandaise del l' Etre*. Brussels: Academic Royale des Sciences Colonials.

Kajosi, S. (2013). *Suala la Uzazi katika Ontolojia ya Kibantu na Jinsi Lilivyojitokeza katika Riwaya za Kiswahili* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Kasprisin, L. (1987). Literature as a Way of Knowing: An Epistemological Justification for Literary Studies. *Journal of Aesthetic Education*, 21(3):17-27. Inapatikana katika https://doi.org/10.2307/3332867.

Kavishe, R.A. (2019). *Ujitokezaji wa Falsafa ya Ubuntu katika Riwava ya Kiswahili: Uchunguzi wa Adili na Nduguze (1952) na Siku ya Watenzi Wote (1968)* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Kiango, S.D. (1973). Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili Upande wa Michezo ya Kuigiza. *Kiswahili*, 43(2), 88-96.

Kitereza, A. (1980). *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka na Ntulanalwo na Bulihwali Juzuu ya 1*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Louw, J.D. (h.t). Ubuntu: An African Assessment of the Religious Other. Inapatikana katika https://www.bu.edu/wcp/Papers/Afri/AfriLouw.htm.

Madumulla, J.S. (1988). Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka. *Kiswahili*, 55, 182-195.

Mbiti, J. (2011). *Introduction to African Religion*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mbiti, J.S. (1995). *African Religion and Philosophy*. London: Heinemann.

Mlacha, S.A.K. (1996). Utamaduni wa Mwafrika katika Riwaya ya Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka. *Mulika*, 23, 24-35.

Newman, L. (2023). Descartes' Epistemology. In E.N. Zalta, & U. Nodelman (Eds.), *The Stanford Encyclopedia of Philosophy (2023 edition)*. Inapatikana katika https://plato.stanford.edu/archives/.

Ndaba, W.J. (1994). *Ubuntu in Comparison to Western Philosophies*. Pretoria: Ubuntu School of Philosophy.

Obenga, T. (2004). Ancient History of African Philosophy. Katika K. Wiredu (Mh.) *A Comparison to African Philosophy* (kur. 31-35). Cambridge: Blackwell Publishing Ltd.

Omari, C. (1980). Utamaduni na Jamii. *Katika Mitaala ya Lugha na Fasihi, Urithi na Utamaduni Wetu*. Na. 9. Dar es Salaam: TPH.

Onyedinma, E.E. & Kanayo, L.N. (2013). "Understanding Human Relations in African Traditional Religious Context in the Face of Globalization: Nigerian Perspectives". *American International Journal of Contemporary Research*. Inapatikana katika https://aijcrnet.com/journals/Vol._3_No._2_February_2013/7.

Oruka, H.O. (1990). *Trends in Contemporary African Phylosophy*. Nairobi: Shirikon Publishers.

Ponera, A. (2023). Uchimuzi wa Epistemolojia ya Wabantu kuhusu Ontolojia ya Mtu katika Riwaya ya Shaaban Robert. *Mulika*, 42(2), 197-216. doi.org/10.56279/mulika.na 42t2.4.

Ponera, A. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Prinsloo, E.D. (1995). *Ubuntu from a Eurocentric and Afrocentric Perspective and its Influence on Leadership*. Pretoria: Ubuntu School of Philosophy.

Ramose, M. B. (2002). *African Philosophy Thought of Ubuntu*. Harare: Mond Books Publishers.

Shutte, A. (1993). *Philosophy for Africa*. Rondebosch: UCT Press

Stumpf, S.E. & Abel, D.C. (2002). *Elements of Philosophy: An Introduction*. New York: McGraw Hill.

Tempels, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

Van Niekerk, A. (1994). *Ubuntu and Religion*. Pretoria: Ubuntu School of Philosophy.

Wamitila, K. W. (2016). *Kamusi Pevu ya Kiswahili*. New Delhi: Vide-Muwa Publishers.

Wiredu, K. (1980). *Philosophy and an African Culture*. Cambridge: Cambridge University Press.